JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

40 Barabara ya Mavuno,
S. L. P 273,
55103, Rukwa.

Barua pepe: rbcrukwa@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113

TAARIFA KWA UMMA

Rukwa
AGOSTI,2024

TAKUKURU RUKWA YASHIRIKISHA WANANCHI KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA KWENYE MIRADI YA MAENDELEO YENYE THAMANI YA SH. 784,200,000

Katika kipindi cha Mwezi Aprili hadi Juni, 2024, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 kupitia madawati ya Uzuiaji Rushwa, Elimu kwa Umma pamoja na Uchunguzi na Mashtaka.

1. UZUIAJI RUSHWA

1.1 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika kipindi hiki, tumefuatilia utekelezaji wa miradi nane (08) ya maendeleo yenye thamani ya shilingi **784,200,000** (Shilingi milioni mia saba themanini na nne laki mbili tu) ili kujua kama kweli fedha iliyotumika inalingana na kazi iliyofanyika. Baadhi ya miradi ilikutwa na kasoro ndogondogo na hatua mbalimbalizimechukuliwa ili kukabiliana na kasoro hizo. Kwa ufafanuzi zaidi rejea **Kiambatisho 1.**

1.2 CHAMBUZI ZA MFUMO:

Kwa upande wa chambuzi za mifumo tunaendelea na uchambuzi wa mifumo mbalimbali hasa ya utoaji wa huduma kwa wananchi ili kubaini mianya ya rushwa na kisha kuweka njia za kuiziba. Kwa mwezi Aprili hadi Juni 2024 tumefanya chambuzi mbili (2) kama ifuatavyo:

- Warsha za uchambuzi wa mfumo wa uagizaji, upokeaji, utunzaji na utoaji wa dawa na vifaa tiba katika halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Katika Warsha hizi mapendekezo kadhaa yaliazimiwa na mapendekezo hayo yameshatekelezwa na ofisi ya MD na DED. (yapi yalibainika na mapendekezo gani yaliyowekwa ambayo yametekelezwa? Yawekwe kwenye jedwali Kiambatisho Na. 2)
-
- Warsha za uchambuzi wa mfumo wa kubaini mianya ya rushwa katika matumizi ya fedha za Elimu bila Malipo katika halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Katika Warsha hizi mapendekezo kadhaa yaliazimiwa na mapendekezo hayo yameshatekelezwa na ofisi ya MD na DED. (yapi yalibainika na mapendekezo gani yaliyowekwa ambayo yametekelezwa? Yawekwe kwenye jedwali Kiambatisho Na. 2)
- Uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa sheria ndogo za afya na usafi wa mazingira katika halmashauri ya Wilaya ya Kalambo
    - Lengo kuu la uchambuzi huu ni kubaini mianya ya rushwa katika mfumo wa usimamizi wa sheria ndogo za afya na usafi wa mazingira katika halmashauri ya Wilaya ya Kalambo. (nini kilibainika na kwenye warsha kama ilifanyika mikakati gani iliwekwa?)

2. ELIMU KWA UMMA

Katika kuhakikisha kwamba Wananchi wa rika na kada mbalimbali katika Mkoa wa wetu wanaendelea kupewa elimu na uelewa juu ya vitendo vya Rushwa, ili washiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya Rushwa ndani ya jamii yetu, tumeendelea na kazi ya uelimishaji umma kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambapo katika kipindi hiki zimefanyika semina ishirini na nne (24) katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Wilaya za Nkasi na Kalambo.

Aidha katika kipindi hiki ofisi imeimarisha klabu za wapinga rushwa hamsini na sita (56) katika Mkoa wa Rukwa na Halmashauri zake kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya kati. Pia TAKUKURU Rukwa na wilaya zake imefanya mikutano ya hadhara ishirini na tisa (29) katika wilaya zake.

3. UCHUNGUZI NA MASHTAKA

(i) Taarifa zilizopokelewa.

Katika kipindi hiki, tumepokea jumla ya taarifa sitini na mbili (62); kati ya hizo, taarifa 49 zilihusu rushwa ambapo ofisi inaendelea kuzifanyia kazi na uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali.

Taarifa 13 kati ya 62 zilizopokelewa hazikuhusu rushwa, hivyo ofisi imetoa ushauri kwa watoa taarifa na kuwaelekeza mahali sahihi pa kuwasilisha malalamiko hayo na hakukuwa na taarifa iliyohamishiwa idara nyingine.

Taarifa hizi zimepokelewa Kisekta katika mchanganuo ufuatao:

IDARA/SEKTA	SUMBAWANGA	KALAMBO	NKASI	JUMLA
Serikali za mitaa/vijiji	1	1	2	4
Elimu	3	6	3	12
Afya	2	2	1	5
Ardhi	2	4	1	7
Polisi	1	3	1	5
Mapato	1	1	0	2
Binafsi	4	3	1	8
Ujenzi	3	1	2	6
ushirika	3	3	3	9
Utumishi	1	2	1	4
Jumla	**21**	**26**	**15**	**62**

(ii) Mashtaka.

Katika kipindi hiki jumla ya kesi kumi na tano (15) ziliendelea katika mahakama mbalimbali za ambapo kati ya hizo kesi mpya ni nane (08). **UTEKELEZAJI WA TAKUKURU RAFIKI**

Utekelezaji wa Programu ya TAKUKURU RAFIKI umeendelea katika kata tano (05) ambazo ni Mpwawa (Sumbawanga DC), Matanga (Sumbawanga Manispaa), Nkandasi, Sintali na Paramawe (Nkasi DC) ambapo wananchi na wadau mbalimbali walitoa kero zao na TAKUKURU (M) Rukwa na wilaya zake kwa kushirikiana na wadau watoa huduma tunaendelea na za utatuzi wake.

4. USHIRIKIANO NA WADAU KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

Katika kipindi cha Mwezi Aprili hadi Juni 2024 tumeendelea kushirikiana na wadau katika kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi.

Aidha, kwa kipindi cha Julai – Septemba, tumejipanga kukabiliana na vitendo vya rushwa katika uchaguzi kwa kufanya yafuatavyo;

ELIMU KWA UMMA

- Kuendelea kufanya semina kwa makundi mbalimbali kama vile vijana, vyama vya siasa, viongozi wa serikali na dini, wafanyabiashara nk
- Kuendelea na programu ya TAKUKURU rafiki ili kuwafikia wadau wengi zaidi
- Kutumia mabanda ya maonyesho wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa na kugawa vipeperushi.

UZUIAJI RUSHWA

- Kufanya tafiti ili kubaini mianya ya rushwa katika maeneo mbalimbali na kushauri idara au taasisi husika namna ya kuziba mianya hiyo kwenye warsha za wadau husika tunazoziandaa.

- **UCHUNGUZI NA MASHTAKA**

- Kupokea taarifa za rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi na kufanya uchunguzi na pale inapobidi kuwachukulia hatua za kisheria watakaokutwa na hatia.

5. TATHMINI YA KAZI KWA MWAKA 2023/24 NA MIKAKATI YA MWAKA 2024/25:

TAKUKURU Rukwa imeshirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kupitia madawati yake ya Uzuiaji, elimu kwa umma na uchunguzi na kwa kupitia programu ya TAKUKURU Rafiki.

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa kupitia Dawati la Uzuaji Rushwa itaendelea kufanya ufuatiliaji wa fedha zinazotolewa na Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa na kudhibiti upoteaji wa fedha za Serikali katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Aidha, kwa upande wa Uelimishaji Umma, tutaendelea kuzielimisha Kamati simamizi za miradi kuhusu uzingatiaji wa miongozo na Sheria ya Manunuzi ya Umma, pamoja na utekelezaji wa Programu ya TAKUKURU RAFIKI ili kupanua wigo kuzuia vitendo vya rushwa visitokee.

WITO:

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa inaendelea kutoa rai kwa wananchi kuendelea kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao na pale wanapobaini uwepo wa ufujaji wa fedha au vifaa vya miradi hiyo basi watoe taarifa kwenye ofisi zetu, ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa tunaendelea kutoa shukrani kwa viongozi mbalimbali na wananchi kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa zinazohusu vitendo vya rushwa.

Aidha, tunawashukuru sana wanahabari wote katika Mkoa wetu wa Rukwa ambao mmekuwa mstari wa mbele kufikisha elimu hii ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi wa wetu na maeneo mengine, maana jukumu la kuzuia rushwa si

la TAKUKURU pekee bali linamhusu kila mtu na kila Mtanzania, na ndiyo maana tunasema

"KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE JUKUMU LETU"

Imetolewa na:

Mzalendo Widege,
Mkuu wa TAKUKURU (M) RUKWA.
0738150186

KIAMBATA NA. 1 MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEMBELEWA

UDHIBITI NA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika kipindi cha mwezi Mei 2024 hadi mwezi Juni 2024 Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imefuatilia na kukagua miradi mitano (05) ya maendeleo yenye thamani ya **Tshs. 609,800,000/=** kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini.

Na.	JINA LA MRADI	THAMANI YA MRADI	HATUA YA MRADI / TATIZO
1.	Uboreshaji wa miundombinu ya kujifunza na kujifunzia katika shule ya Sekondari Chisenga (Mradi wa Barrick Tanzania awamu ya II), halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	Tshs. 430,000,000/=	Mradi upo katika hatua za awali za ujenzi ambazo ni ujenzi wa msingi katika majengo yote ya mradi. Ukaguzi ulibaini kuwa fundi anajenga kwa kutofuata michoro na ramani za msingi hivyo basi, TAKUKURU (W) Kalambo imetoa mapendekezo kwa Mkurugenzi kuhakikisha marekebisho hayo yanafanyika na utekelezaji wa mapendekezo hayo uwasilishwe TAKUKURU (W) Kalambo kwa ajili ya ufuatiliaji.
2.	Ujenzi wa kichomea taka katika zahanati ya Mwimbi.	Tshs. 13,000,000/= Mradi unatekelezwa kwa mfumo wa "Force Account".	Ujenzi umekamilika. TAKUKURU (W) Kalambo imeshauri wasimamizi wa zahanati hii kuzingatia matumizi sahihi ya miundombinu ya mradi huu.

3.	Ujenzi wa kichomea taka katika zahanati ya Ulimi.	Tshs. 13,000,000/= Mradi unatekelezwa kwa mfumo wa "Force Account".	Ujenzi umekamilika. TAKUKURU (W) Kalambo imeshauri wasimamizi wa zahanati hii kuzingatia matumizi sahihi ya miundombinu ya mradi huu.
4.	Ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa na matundu 08 ya choo katika shule ya Sekondari kanda (Mradi wa SEQUIP), halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.	Tsh. 114,400,000/= Mradi unatekelezwa kwa mfumo wa "Force Account".	Mradi upo katika hatua mbalimbali za umaliziaji. Kwa upande wa vyumba vya madarasa vipo katika hatua za kupiga plaster, kufunga gypsum board, kufanya skimming kuta za ndani, na kuweka mifumo ya umeme. Kwa upande wa vyoo vipo katika hatua ya upigaji wa plaster, mashimo ya maji taka yamekamilika pia. Ukaguzi ulibaini ushirikiano hafifu kutoka kwa wataalam wa halmashauri ya manispaa Sumbawanga na Kamati za mradi huu pindi kamati zinapohitaji huduma za kitaalam kutoka kwa wataalam wa Manispaa hali inayopunguza kasi ya ujenzi wa mradi huu. Hivyo basi, TAKUKURU (M) Rukwa imemshauri Mkurugenzi ahakikishe team yake ya wataalam

			inatoa ushirikiano mzuri wa kitaalam kwa kamati za mradi huu ili mradi uweze kukamilika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa.
5.	Ujenzi wa chumba 01 cha darasa na matundu 08 ya choo katika shule ya sekondari Makuzani (Mradi wa SEQUIP), halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.	Tsh. 39,400,000/= Mradi unatekelezwa kwa mfumo wa "Force Account".	Mradi upo katika hatua ya upauaji na umaliziaji Kwa upande wa chumba cha darasa kipo katika hatua za kupiga plaster na upauaji. Kwa upande wa vyoo vipo katika hatua ya ujengaji wa maboma, uchimbaji wa mashimo ya maji taka umekamilika na upo katika hatua ya ujengeaji. Mradi umechelewa kuanza kutokana na changamoto ya upatikanaji wa matofali kwa hiyo kamati ya shule iliazimia kukodi mashine ya kufyatulia matofali ya block na kazi ya kufyatua tofali hizo inafanyika hapo hapo eneo la mradi hali inayopunguza kasi ya utekelezaji wa mradi. Mradi hauna "Issue Voucher", kwa

			hiyo inapelekea utunzaji mbovu wa kumbukumbu za utoaji wa vifaa katika stoo ya mradi, hivyo TAKUKURU (M) imeshauri wasimamizi wa mradi kuhakikisha wanakuwa na "Issue voucher" ili kuhakikisha utunzaji mzuri wa kumbukumbu za vifaa vinavyotoka stoo. Ufuatiliaji huu pia umebaini kuwa Mkuu wa shule anapokea maelekezo kutoka kwa wataalam wa halmashauri ambayo hayako katika maandishi hali inayopelekea baadhi ya kazi kufanyika kinyume na mwongozo wa mradi tajwa.
JUMLA		**Tshs. 609,800,000/=**	

CHAMBUZI *ZA MFUMO:*

TAKUKURU Mkoa wa Rukwa tunaendelea na uchambuzi wa mifumo mbalimbali hasa ya utoaji wa huduma kwa wananchi ili kubaini mianya ya rushwa na kisha kuweka njia za kuiziba. Kwa mwezi Mei 2024 hadi June 2024 tumefanya chambuzi mbili (2) kama ifuatavyo:

- Warsha za uchambuzi wa mfumo wa uagizaji, upokeaji, utunzaji na utoaji wa dawa na vifaa tiba katika halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na

Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Katika Warsha hizi mapendekezo kadhaa yaliazimiwa na mapendekezo hayo yameshatekelezwa na ofisi ya MD na DED.

- Warsha za uchambuzi wa mfumo wa kubaini mianya ya rushwa katika matumizi ya fedha za Elimu bila Malipo katika halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Katika Warsha hizi mapendekezo kadhaa yaliazimiwa na mapendekezo hayo yameshatekelezwa na ofisi ya MD na DED.
- Uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa sheria ndogo za afya na usafi wa mazingira katika halmashauri ya Wilaya ya Kalambo
    - Lengo kuu la uchambuzi huu ni kubaini mianya ya rushwa katika mfumo wa usimamizi wa sheria ndogo za afya na usafi wa mazingira katika halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

TAKUKURU RAFIKI:

Utekelezaji wa Programu ya TAKUKURU RAFIKI umeendelea katika kata tano (05) ambazo ni Kata ya Mpwapwa (SDC), Kata ya Matanga (SMC), Kata ya Nkandasi, Kata ya Simtali na Kata ya Paramawe halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ambapo wananchi na wadau mbalimbali wametoa kero zao na TAKUKURU (M) Rukwa kwa kushirikiana na wadau watoa huduma tunaendelea na hatua za utatuzi wake.

Naomba kuwasilisha.

TAARIFA YA UZUIAJI RUSHWA TAKUKURU (W) KALAMBO KWA MWEZI APRILI, 2024

MIRADI YA MAENDELEO

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 TAKUKURU Wilaya ya Kalambo imefuatilia na kukagua miradi mitatu(03) ya maendeleo kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Na.	KAZI ZILIZOFANYIKA	THAMANI YA MRADI	HATUA YA MRADI
01.	Umaliziaji wa chumba cha maabara 1 shule ya Sekondari Kasanga	Tsh. 30,000,000/=	Umaliziaji upo katika hatua za upakaji rangi na upachikaji wa madirisha ya "Aluminium". Mfumo wa gesi na maji bado haujakamilika. Eneo la kutunzia gesi (Gas Chamber) linaendelea kujengwa.
02.	Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa na matundu 8 ya vyoo Shule ya Sekondari Kasanga	Tsh. 114,400,000/=	Ujenzi wa maboma upo katika hatua ya msingi. Uchimbaji wa mashimo ya majitaka unaendelea
03.	Ujenzi wa uzio wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Msanzi	Tsh.30,000,000/=	Ujenzi wa kuta unaendelea.
JUMLA		**174,400,000/=**	